Tangazo la Serikali Na. …………………. la tarehe …………………..

# SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI

## SURA YA 413

## KANUNI ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA UKAGUZI WA LAZIMA WA VYOMBO VYA USAFIRISHAJI KIBIASHARA ZA MWAKA, 2023,

## MPANGILIO WA KANUNI

### SEHEMU YA KWANZA
### VIFUNGU VYA AWALI

Kanuni Jina

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

### SEHEMU YA PILI
### UKAGUZI WA LAZIMA WA CHOMBO

4. Ukaguzi wa lazima wa chombo
5. Ada ya ukaguzi.
6. Kituo cha ukaguzi.
7. Hatua za ukaguzi

### SEHEMU YA TATU
### VIWANGO VYA UKAGUZI WA CHOMBO

8. Ukaguzi wa chombo.
9. Makundi ya ukaguzi wa chombo.
10. Aina za ukaguzi wa chombo.
11. Usalama na uhakiki wa chombo.

12. Kipimo cha utoaji hewa ukaa wa chombo.
13. Moshi unaoonekana.
14. Kiwango cha kelele.
15. Uteuzi wa mkaguzi wa chombo.
16. Mamlaka ya mkaguzi aliyeidhinishwa.
17. Wajibu wa mkaguzi aliyeidhinishwa
18. Wajibu wa mtoa huduma
19. Ukaguzi na uthibitishaji wa chombo.

SEHEMU YA NNE
UKAGUZI NA UTHIBITISHAJI WA CHOMBO
KWA AJILI YA MATUMIZI BARABARANI

20. Uzingatiaji usalama wa chombo.
21. Chombo kisichoweza kuthibitishwa kwa matumizi ya barabara.
22. Mapitio.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA JUMLA

23. Makosa na adhabu.
24. Wajibu wa mtoa huduma aliyethibitishwa.
25. Mapungufu, kuharibika na mabadiliko ya chombo.
26. Mamlaka ya kusimamisha chombo.

MAJEDWALI

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI

(SURA YA 413)

---

**KANUNI**

---

*(Zimetengenezwa chini ya Kanuni 45(2))*

---

KANUNI ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA UKAGUZI WA LAZIMA WA VYOMBO VYA USAFIRISHAJI KIBIASHARA ZA MWAKA, 2023

SEHEMU YA KWANZA
VIFUNGU VYA AWALI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za Ukaguzi wa Lazima wa Vyombo vya Usafirishaji Kibiashara za mwaka, 2023.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika kwa vyombo vinavyotoa huduma za usafirishaji kibiashara.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo-

Sura ya 413

"sheria" maana yake ni Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini;

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria;

"mkaguzi aliyethibitishwa" maana yake ni mtu aliyeteuliwa na Mamlaka kama mkaguzi chini ya Kanuni hizi;

"cheti cha ubora wa chombo" maana yake ni cheti cha kuthibitisha ubora wa chombo kutumika barabarani kinachotolewa chini ya Kanuni hizi;

" chombo cha usafirishaji kibiashara" maana yake ni chombo cha moto kilichotengenezwa au kinachotumika kutoa huduma ya usafirishaji kibiashara;

"viwango vya hewa ukaa" maana yake ni kiwango cha hewa ukaa kinachokubalika kutoka kwenye chombo cha moto kwenye mazingira;

"ukaguzi" maana yake ni ukaguzi wa chombo unaofanyika kwa mujibu wa Kanuni hizi;

"kituo cha ukaguzi" maana yake ni kituo kilichoanzishwa kwa ukagauzi wa lazima wa magari na

inajumuisha vituo vinavyo hama;

"Ukaguzi wa lazima wa chombo" maana yake ni utaratibu uliowekwa na Mamlaka wa ukaguzi wa chombo ili kuhakikisha kuwa kinakidhi masharti ya Kanuni hizi;

“mabadiliko" maana yake ni kufanya mabadiliko ya chombo kutoka katika hali yake ya awali kwa kubadilisha, kuongeza au kuondoa muundo, mfumo, sehemu au vifaa lakini haijumuishi ukarabati; na

“mtoa huduma” maana yake ni mtu ambaye anamiliki chombo cha usafirishaji kibiashara.

## SEHEMU YA PILI
## UKAGUZI WA LAZIMA WA CHOMBO CHA USAFIRISHAJI KIBIASHARA

Ukaguzi wa lazima wa chombo

4. (1) mtoa huduma wa chombo cha usafirishaji kibiashara atahakikisha kuwa chombo kinakaguliwa angalau kila baada ya miezi sita katika kituo cha ukaguzi kilichoidhinishwa.

(2) endapo mtoa huduma atahitaji chombo chake kikaguliwe katika makubaliano binafsi, Mamlaka itakagua chombo kwa gharama ya mtoa huduma.

Ada ya ukaguzi

5. Mtoa huduma atatakiwa kulipa ada ya ukaguzi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza katika Kanuni hizi.

Kituo cha ukaguzi

6. (1) Mamlaka, kwa madhumuni ya Kanuni hizi itaanzisha, kuidhinisha au kuteua vituo vya ukaguzi wa vyombo, kadili itakavyoona inafaa.

(2) vituo vya ukaguzi katika Kanuni hizi vinaweza kumilikiwa na:

(a) serikali;
(b) mashirika ya umma;
(c) taasisi binafsi; au
(d) katika utaratibu wa ubia kati ya umma na sekta binafsi.

Hatua za ukaguzi

7. Ukaguzi wa chombo utafanyika katika hatua zifuatazo:

(a) Utambuzi wa chombo ili kuhakikisha chombo sahihi kinakaguliwa;
(b) ukaguzi wa awali wa ndani na nje ya chombo; na
(c) upimaji kwa kutumia mitambo.

## SEHEMU YA TATU
## VIWANGO VYA UKAGUZI WA CHOMBO

Ukaguzi wa chombo

8. Chombo cha moto kilichowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi wa lazima kitafanyiwa ukaguzi kwa macho na kwa kutumia mitambo katika vipengere vilivyoainishwa chini ya Jedwali la Tatu la Kanuni hizi.

Makundi ya ukaguzi wa chombo

9. Kutakuwa na makundi matatu ya ukaguzi wa chombo-

(a) kundi A, ukaguzi wa kawaida wa lazima utakaofanyika mara mbili kwa mwaka;
(b) kundi B, ukaguzi unaofanyika kwa maombi ya mtoa huduma; na
(c) kundi C, ukaguzi unaofanyika kwa amri ya mahakama au chombo chenye mamlaka;

Aina za ukaguzi wa chombo

10. (1) Kutakuwa na aina sita za ukaguzi wa chombo-

(a) ukaguzi wa awali wa chombo unaofanyika kwa chombo kilichosajiliwa kwa mara ya kwanza kwa ajili ya kutoa huduma za usafiri kibiashara;
(b) ukaguzi wa kipindi maalum unaofanyika kwa chombo baada ya kuisha kwa muda wa cheti cha ukaguzi wa awali;
(c) ukaguzi wa chombo unafanyika baada ya kufanya mabadiliko ya kubadili urefu, upana na marekebisho mengine yaliyofanyika;
(d) ukaguzi wa chombo unaofanyika baada ya ajali;
(e) ukaguzi wa chombo unaofanywa wakati au baada ya kubadilisha umiliki; na
(f) ukaguzi wa barabarani.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1) (d), pale ambapo chombo chenye cheti cha ubora wa kutumika barabarani kimehusika kwenye ajali, kitatakiwa kukaguliwa na mkaguzi aliyeidhinishwa ambaye atatoa amri ya kurudia ukaguzi baada ya matengenezo ili kujiridhisha na ubora wa chombo hicho.

Usalama na uhakiki wa chombo

11. (1) Ukaguzi wa chombo utafanyika ili kupima usalama na kujiridhisha na vipengele au maeneo yaliyoainishwa kwenye Jedwali la pili la Kanuni hizi.

(2) Endapo kipengele chini ya kanuni ndogo ya (1) kina viwango vya Kitaifa kama ilivyoainishwa kwenye sheria husika, kipimo katika eneo hilo kitapaswa kuzingatia viwango hivyo.

(3) Bila kuathiri kipengele au eneo katika Jedwali la pili la Kanuni hizi, kipimo kinaweza kufanywa kwenye kipengele au eneo linguine endapo jaribio hilo limeidhinishwa na mamlaka husika.

Kipimo cha utoaji hewa

12. (1) Chombo kitakuwa katika hali inayozingatia viwango vya utoaji wa hewa ukaa katika

ukaa wa chombo

daraja la chombo na aina ya mafuta ya chombo iliyoidhinishwa na mamlaka.

(2) Ukaguzi wa uzalishaji wa hewa ukaa wa chombo utafanyika kwa pamoja na ukaguzi wa usalama.

(3) Chombo kilichowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi wa uzalishaji wa hewa ukaa kitafanyia vipimo vya uunguzaji wa mafuta ya injini inayotumia.

Moshi unaoonekana

13. Chombo hakitatakiwa kutoa moshi unaoonekana wazi wakati injini ya chombo ikiwa inafanya kazi katika hali ya joto la kawaida.

Kiwango cha kelele.

14. (1) Kila chombo cha moto kitakaguliwa kupima kiwango cha kelele kinachozalisha.

(2) Kifaa cha kuzuia sauti ya chombo cha moto kwenye mfumo wa kutolewa hewa hakitakiwi kuwa na kutu, uharibifu na kupasuka ili kudhibiti sauti inayotoka kuzuia kelele.

(3) Kipimo cha kiwango cha kelele cha injini inayofanya kazi na kelele katika kichwa cha chombo itaendana na viwango vilivyowekwa na mamlaka ya husika ya kushughulikia viwango.

Uteuzi wa mkaguzi wa chombo

15. Kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi chini ya Kanuni hizi, Mamlaka inapaswa kuteua Mkaguzi aliyeidhinishwa au kukaimisha mamlaka ya ukaguzi wa lazima wa chombo kwa taasisi nyingine.

Mamlaka ya mkaguzi aliyeidhinishwa

16. Mkaguzi aliyeidhinishwa, katika kutekeleza majukumu yake atakuwa na mamlaka ya kufanya yafuatayo-

(a) kumtaka mwendesha chombo kuzingatia viwango vilivyoainishwakwenye masuala ya ukaguzi;
(b) kutoa mapendekezo au kutoa amri ya kufuta usajili wa chombo ambacho hakikidhi viwango vilivyoainishwa;
(c) kutoa cheti cha kukidhi au kutokukidhi ubora wa chombo kuwepo barabarani;
(d) kuingia katika eneo lililotengwa kwa ajili ya vyombo vya moto kufanya ukaguzi kwa makubaliano binafsi;

Wajibu wa mkaguzi aliyeidhinishwa

17. Mkaguzi aliyeidhinishwa atahakikisha kuwa;

(a) chombo kilichokaguliwa kinafaa kutumika barabarani;
(b) anatoa cheti cha kukidhi au kutokukidhi ubora wa chombo kuwepo barabarani;
(c) ukaguzi wa chombo cha moto unafanyika kwa wakati;
(d) kuwa muadilifu na kutumia weledi wakati wa kutekeleza majukumu yake;
(e) anatunza kumbukumbu za ukaguzi salama na kuziwasilisha kwa mamlaka zitakapohitajika;

(f) anazingatia viwango vya ukaguzi wa chombo; na

(g) kituo cha ukaguzi kina vifaa, nyenzo na wafanyakazi stahiki.

Wajibu wa mtoa huduma

18. (1) kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi, mtoa huduma atahakikisha kuwa-

(a) chombo ni kisafi kumuwezesha mkaguzi kukagua sehemu zote;
(b) vimiminika havimwagiki kupita kiasi.
(c) chombo ni salama kuendeshwa;
(d) taarifa za chombo hazijachezewa;
(e) ada stahiki inalipwa; na
(f) kadi ya usajili wa chombo inatolewa inapohitajika.

## SEHEMU YA NNE
## UKAGUZI NA UTHIBITISHAJI WA CHOMBO KWA MATUMIZI YA BARABARANI

Ukaguzi na uthibitishaji wa chombo

19. (1) Ukaguzi wa chombo kwa ajili ya matumizi ya barabara utafanyika na mkaguzi aliyeidhinishwa.

(2) Mkaguzi aliyeidhinishwa, baada ya ukaguzi wa chombo-

(a) atatoa cheti cha ubora wa chombo kutumika barabarani kwa chombo kinachokidhi; au

(b) atatoa cheti cha kutokukidhi kwa chombo kisichokidhi kutumika barabarani;

(3) Endapo mkaguzi aliyeidhinishwa wakati wa kukagua chombo chini ya Kanuni hizi, atabaini kuwa chombo hakikidhi masharti ya sheria zinazohusu masuala ya usalama barabarani, ataandaa orodha ya mapungufu yote yaliyobainika na kumpatia mtoa huduma nakala ya orodha hiyo na atamtaarifu tarehe ambayo mapungufu hayo yanapaswa kuwa yamerekebishwa na kurudisha chombo kwa ajili ya ukaguzi.

Uzingatiaji usalama wa chombo

20. Chombo kinaweza kuthibitishwa kwaa ajili ya matumizi barabarani endapo mkaguzi aliyethibitishwa atajiridhisha kuwa chombo-

(a) ni salama kwa matumizi;

(b) kipo katika hali ya uhimilivu kiusalama baada ya kutengenezwa au kubadilishwa; na

(c) kimefanyiwa ukaguzi wa lazima kwa mujibu wa Kanuni hizi.

Chombo kisichoweza kuthibitishwa kwa matumizi ya barabara

21. chombo hakitathibitishwa kutumika barabarani ikiwa-

(a) kimefutiwa usajili;
(b) maombi ya kubadilisha matumizi ya chombo yamefanyika; na
(c) kimefanyiwa mabadiliko yanayothiri usalama wa ufanyaji kazi wake.

Mapitio TS. Na. 73 la 2020

22. Mtu ambaye hajaridhika na maamuzi ya Mkaguzi aliyethibitishwa chini ya Kanuni hizi atatakiwa kuwasilisha maombi ya mapitio kwa maandishi kwa mujibu wa Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini za Utaratibu wa Mapitio, 2020.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA UJUMLA

Makosa na adhabu

23. (1) Mtu ambaye atashindwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi ametenda kosa na atapopatikana na hatia atawajibika-

(i) ikiwa ni kosa la kwanza, atalipa faini isiyopungua shilingi laki tano na isiyozidi shilingi milioni moja; na

(ii) ikiwa ni kosa la pili au zaidi, atalipa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi Shilingi milioni tatu au kifungo muda usiopungua miezi mitatu jela lakini usiozidi miezi sita au vyote.

(2) Pasipo kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Mamlaka inaweza kumsimamisha mkaguzi aliyethibitishwa katika majukumu yake.

Wajibu wa mtoa huduma aliyethibitishwa

24. (1) Mtoa huduma wa chombo chenye cheti cha ubora wa kutumika barabarani-

(a) atahakikisha kuwa cheti cha ubora wa chombo kutumika barabarani kinakuwa kwenye chombo; na
(b) endapo itahitajika kufanya hivyo, atawasilisha cheti cha ubora wa chombo na nyaraka yoyote inayohusiana na chombo kwa mkaguzi aliyeidhinishwa ndani ya muda ulioainishwa.

(2) Endapo nyaraka iliyotolewa chini ya Kanuni hizi imepotea au kuharibika, mtoa huduma atayakiwa kutoa notisi mapema kwa kituo cha polisi na kuomba kupewa nakala durufu kwa Mamlaka inayohusika.

Mapungufu, kuharibika na mabadiliko ya chombo

25. (1) Endapo mapungufu au uharibifu utatokea kwa chombo ambacho kina cheti cha ubora wa kutumika barabarani kwa mujibu wa Kanuni hizi, na mapungufu au uharibifu huo unaweza kuathiri usalama wa mtu anayetumia chombo, mtumiaji wa barabarani au miundombinu ya barabara, hakitatumika hadi hapo mapungufu yamerekebishwa na cheti kipya cha ubora

kutumika barabarani kimetolewa.

(2) Mabadiliko yoyote yatakayofanywa kwenye chombo chenye cheti cha ubora wa kutumika barabarani kilichotolewa chini ya Kanuni hizi, mtoa huduma wa chombo hicho atatakiwa kukipeleka chombo hicho kwenye kituo cha ukaguzi kwa ajili ya kukaguliwa pindi anapofanya mabadiliko.

Mamlaka ya kusimamisha chombo

26. Mkaguzi aliyeidhinishwa kwa madhumuni ya kutekeleza Kanuni hizi anaweza kwa muda wowote kufanya yafuatayo;

(a) kusimamisha chombo chochote ambacho anahisi kinafanya kazi kikiwa na ubovu au kutokuwa na cheti cha ubora wa kutumika barabarani;

(b) kumtaka mtoa huduma wa chombo-

(i) kutoa cheti cha ubora wa kutumika barabarani au nyaraka yoyote inayohusiana na chombo; na

(ii) kuwasilisha chombo kwa ajili ya ukaguzi katika muda na mahali kinapotakiwa.

## JEDWALI LA KWANZA

### ADA ZA UKAGUZI WA CHOMBO

(Zimetengenezwa chini ya Kanuni ya 5)

| NAMBA | AINA YA CHOMBO | ADA YA UKAGUZI | ADA YA UKAGUZI MWINGINE |
|---|---|---|---|
| 1. | Pikipiki za magurudumu mawili | 10,000/= | 10,000/= |
| 2. | Pikipiki za magurudumu matatu | 15,000/= | 15,000/= |
| 3. | Magari ya abiria – 4 -15 | 20,000/= | 20,000/= |
| 4. | Magari ya abiria - 16-25 | 30,000/= | 30,000/= |
| 5. | Magari ya abiria - 26-45 | 50,000/= | 50,000/= |
| 6. | Magari ya abiria - 46- 60 | 70,000/= | 70,000/= |
| 7. | Magari ya abiria - 61- na kuendelea | 90,000/= | 90,000/= |
| 8. | Magari ya kazi nyepesi. – 3500kg | 50,000/= | 50,000/= |
| 9. | H.C.V. +3500kg | 70,000/= | 70,000/= |
| 10. | Tela (-35000kg) | 60,000/= | 60,000/= |
| 11. | Tela (+35000kg) | 70,000/= | 70,000/= |

JEDWALI LA PILI

VIWANGO VYA UKAGUZI WA CHOMBO

(Zimetengenezwa chini ya kanuni 11(1))

| **Na.** | **KIFAA** | **WIGO WA UKAGUZI** | **MAPENDEKEZO** | |
|---|---|---|---|---|
| | | | **NZURI** | **HATARISHI** |
| 1 | HALI YA MAGURUDUMU | ULIKAJI/ KUTOKEZA NYUZI AU WAYA/KUISHA KWA MUDA WA MATUMIZI | | |
| 2 | GURUDUMU LA ZIADA/ JACK NA MKONO | VYOTE VIPO/KUWA NA HALI NZURI | | |
| 3 | MKANDA WA FENI NA WA KIYOYOZI | VIMEFUNGWA NA VIPO KWENYE HALI NZURI/ | | |
| 4. | OILI YA INJINI | KAGUA UJAZO/HALI YA KUVUJA/UWEPO WA CHEMBECHEMBE/RANGI | | |
| 5. | UJAZO WA MAJI/REJETA | UJAZO SAHIHI/HALI YA KUVUJA | | |
| 6. | HALI KIMIMINIKA CHA USUKANI | UJAZO SAHIHI/HALI YA KUVUJA | | |
| 7. | GEJI YA MAFUTA | KAMA INAFANYA KAZI | | |
| 8. | MAFUTA YA BREKI | UJAZO SAHIHI/HALI YA KUVUJA/AINA YA MAFUTA YALIYOPENDEKEZWA | | |
| 9. | HALI YA BETRI | HALI YA CHAJI/KIASI CHA MAJI/HALI YA VIUNGO | | |
| 10. | KIFUTA MAJI/KIOO CHA MBELE | KIPO/KINAFANYA KAZI | | |
| 11. | HONI | INAFANYA KAZI | | |
| 12. | TAA ZA MBELE,/ TAHADHARI,/ BREKI,/TAA ZA KUEGESHA | HALI YA KUFANYA KAZI/NAMNA YA KUTAWANYA MWANGA | | |
| 13. | HALI YA MUONEKANO WA CHOMBO KWA UJUMLA | MUONEKANO MZURI NA HAKUNA HITILAFU KUBWA | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 14. | KIFAA CHA TAHADHARI YA MOTO | KINAFANYA KAZI NA KIPO SEHEMU SAHIHI/MUDA WA KUISHA MATUMIZI | | |
| 15 | KIOO CHA NDANI/NJE PEMBENI/KIOO CHA MBELE | VIPO KWENYE HALI NZURI/HAVIJAVUNJIKA | | |
| 16. | BREKI YA MKONO/MGUU KWA AJILI YA KUEGESHA CHOMBO | KAMA ZINAFANYA KAZI | | |
| 17. | MIKANDA YA VITI | KUWA KWENYE HALI NZURI/INAFANYA KAZI | | |
| 18. | ALAMA ZA ONYO | KUWEPO NA KUTOHARIBIKA | | |
| 19. | BREKI YA INJINI | KUFANYA KAZI | | |
| 20. | GEJI ZA UPEPO/ MFUMO WA UPEPO | UNAFANYA KAZI | | |
| 21. | MFUMO WA KUFUATILIA MWENENDO WA GARI | UNAFANYA KAZI | | |

JEDWALI LA TATU

VIWANGO VYA UBORA WA KITUO CHA UKAGUZI

(Zimetengenezwa chini ya Kanuni 8)

| Na. | **VIPIMO** | **VIFAA VYA UKAGUZI** |
|---|---|---|
| 1. | Uthibitisho wa vifaa vya matengenezo na kazi | Kipimo cha mkanda |
| 2. | Vipimo vya uzito | Mita ya uzito |
| 3. | Mlingano wa usawa wa gurudumu | (Upande wa kuingizwa tester) mashine ya kupima mlingano |
| 4 | Mgawanyiko wa uzito wa magurudumu | Mashine ya kupima balansi |
| 5. | Mwonekano wa kioo cha nyuma | Kipimo cha mkanda |
| 5. | Hali ya utendaji wa kupunguza kasi wa mfumo wa breki msaidizi | Kifaa cha kupima kupungua au kifaa cha kupima kasi, saa na kuthibitisha |
| 6. | Utendaji wa breki | Kusimamisha kifaa cha kupimia umbali, kifaa cha kugundua kasi ya gari na msingi wa kutibitisha |
| 7. | Kifaa cha onyo kuhusu kuvuja kwa maji ya breki | Mita ya kiwango cha sauti, kipaza sauti na chombo cha kupimia kiasi cha maji |
| 8. | Kipimo cha kiwango cha kelele inaoendelea | Mita ya kiwango cha sauti, kipaza sauti, kinasa sauti, kifaa cha kugundua kasi ya gari na msingi wa kuthibitisha |
| 9. | Kipimo cha kiwango cha kelele iliyofikia ukomo | Sound level meter, kipaza sauti, kinasa sauti, na msingi wa kuthibitisha |
| 10. | Ukaguzi wa kiwango cha sauti | Mita ya kiwango cha sauti, kipaza sauti, kinasa sauti, tachometer ya injini na msingi wa |

| | | |
|---|---|---|
| | | kuthibitisha. |
| 11. | Ukaguzi wa taa za mbele | mwangaza, kioo na chumba cheusi |
| 12. | Ukaguzi wa taa ya ukungu wa mbele | mwangaza, skrini na chumba cheusi |
| 13. | Kuhusu utendaji wa taa | mwangaza, Skrini, chombo cha kupima pembe na chumba cheusi |
| 14. | Jaribio la kufanya kazi kwa taa kwenye namba ya usajili (nyuma) | Mwangaza na mita ya mwangaza wa mwanga, sampuli ya kiwanda cha majaribio na chumba cheusi. |
| 15. | Jaribio la taa | Illuminometer, screen and dark room |
| 16. | Jaribio la kiwango cha sauti ya honi | Mita ya kiwango cha sauti na kipaza sauti |
| 17. | Jaribio la kipimo cha hewa ukaa inayotolewa wakati injini haina mzigo | Dainamomita ya chasi, kipulizia, kifaa cha kuonyesha ratiba ya kuendesha, skana ya kupima hali ya injini, kinasa sauti, mita ya kasi ya gari, tachometer ya injini, gesi za kumbukumbuku, kipima joto, kipimajoto, hidromita, mita ya mwelekeo wa upepo, kifaa cha kupima gharama ya chini na chumba cha mtihani |
| 18. | Mtihani wa ukolezi wa moshi wa dizeli (3- hali, hakuna kuongeza kasi ya mzigo) | Dainamomita ya chasi na dynamometer ya injini, kifaa cha sampuli ya moshi wa kutolea nje ya blower, kifaa cha kupima ukolezi, kipima kipimo na kipima joto. |
| 19. | Jaribio la kutoa hewa ya ukaa kwa modeli ya diseli 10 - 15 | Dainamomita ya chasi, kipulizia, kifaa cha kuonyesha ratiba ya kuendesha, skana ya kupima hali ya injini, kichanganuzi cha utoaji wa kutolea nje, kinasa sauti, mita ya kasi ya gari, takomita ya injini, gesi za kumbukumbu, barometer, kipima joto, mita ya mwelekeo wa upepo, Manifodi ya kutolea hewa ya ukaa, kishikilia kichujio, pampu ya kunyonya sampuli, safisha mita ya sampuli ya utoaji wa moshi, mizani ya uzito, chumba cha kupimia na |

| | | |
|---|---|---|
| | | chumba cha mtihani. |
| 20. | Jaribio la kutoa hewa ya ukaa kwa modeli ya diseli 6 | Dinamomita ya chasi au dainamomita ya injini, kichanganuzi cha kutolea moshi, kinasa sauti, kifaa cha kupimia kiasi cha ulaji, kifaa cha kupimia matumizi ya mafuta, takomita ya injini, gesi za kumbukumbu, kipima joto na chumba cha mtihani. |
| 21. | Jaribio la kutoa hewa ya ukaa kwa modeli ya diseli 23 | Dainamomita ya chasi au ya injini, kichanganuzi cha kutolea moshi, kinasa sauti, kifaa cha kupimia kiasi cha ulaji, kifaa cha kupimia matumizi ya mafuta, tachometer ya injini, gesi za kumbukumbu, kipima joto na chumba cha kupimia. |
| 22. | Jaribio la madhara ya joto la ziada kwenye injini | Dainomita ya chasi au ya injini, kichanganuzi cha kutolea moshi cha blower, kinasa sauti na chumba cha kupimia. |
| 23. | Jaribio la kiwango cha matumizi ya mafuta kwa modeli ya 10.15 | Dainamomita chasi, kipulizia, kifaa cha kuonyesha ratiba ya kuendesha, skana ya hali ya injini, kichanganuzi cha utoaji wa kutolea nje, kinasa sauti, mita ya kasi ya gari, takomita ya injini, gesi za kumbukumbu, barometer, kipima joto, mita ya mwelekeo wa upepo, bomba la kutolea hewa ya ukaa, kishikilia kichujio, pampu ya kunyonya sampuli, safisha mita ya sampuli ya utoaji wa moshi, mizani ya uzito, chumba cha kupimia. |
| 24. | Uthibitisho wa vifaa vya ujenzi na kazi za gari ambazo zimepitia uimara wa kuendesha | Shimo au kipimo cha mkanda |
| 25. | Kipimo cha hali ya hewa ya ukaa kwa injini isiyo na mzigo baada ya kutembea kwa muda mrefu modeli ya 10 -15 | Dainamita ya chasi, kipulizia, kifaa cha kuonyesha ratiba ya kuendesha, skankupimia hali ya injini, kichanganuzi cha utoaji wa kutolea nje, kinasa sauti, mita ya kasi ya gari, tachometer ya injini, gesi za kumbukumbu, barometer, kipima joto, mita ya mwelekeo wa |

| | | |
|---|---|---|
| | | upepo, bomba la kutolea hewa ya ukaa, kishikilia kichujio, pampu ya kunyonya sampuli, safisha mita ya sampuli ya utoaji wa moshi, mizani ya uzito, chumba cha kupimia na chumba cha mtihani. |
| 26. | Vipimo vingine/ uchunguzi unaoonekana kama ni muhimu | Vifaa muhimu kwa ajili ya mtihani husika |

Imetolewa na

Dodoma, Makame Mbarawa,
………………, 2023 *Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi*